# MTIHANI WA PAMOJA WA SULIMO

**102/2** **KISWAHILI** **LUGHA**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**JULAI 2025**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**UFAHAMU: ( Alama 15)**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Ulikuwa wakati wa jioni jua limepunguza udhia wake na upepo mwanana ulikuwa ukipita na kuzipapasa Ngozi zetu mfano wa pamba. Kama ilivyokuwa desturi yetu pale chuoni, siku hiyo tuliketi karibu na lango kuu la chuo ili kutafiti kazi mradi tuliyokuwa tumepewa darasani. Sehemu hii tuliipenda sana kwa kuwa kuuchakura mtandao ilikuwa ni bure bora tu ufahamu nywila ya mtandao huo. Mandhari ya sehemu hii pia yaliwavutia wanafunzi wengi katika sehemu hii.

Tulipotia fahamu, tulipata mazoea haya yamekita mizizi nasi tukawa hatuna budi kuyakumbatia. Hatukuyakumbatia tu, bali tuliyakumbatia kwa dhati ya moyo. Vikao hivi havikuwa tu hazina kubwa kwetu bali pia vilikuwa vya thamani isiyomithilika. Hapa ndipo tulinoleana bongo kwa kupashana habari. Leo hii tumo katika mjadala kuhusu kuhusu mfumo mpya wa elimu CBC tuliopewa darasani kama kazi mradi. Nahodha wa kikundi hiki anampa msemaji wa kwanza nafasi naye hakusita kushika usukani.

"Nionavyo mimi, mfumo wa CBC unafaa kufutiliwa mbali. Serikali haijajiandaa vilivyo ili kuufanikisha mfumo huu wa elimu. Kwanza, mafunzo waliyopewa walimu ili kuufanikisha mfumo huu kamwe hayatoshi. Nionavyo mimi ni kwamba walimu waliopo ambao idadi yao haitoshi, wanatumia elimu ya mfumo wa 8-4-4 kuufunza ule wa CBC. Itawezekanaje mwalimu apate mafunzo ya wiki moja kisha akawa amefuzu kumwelekeza mwanafunzi? Isitoshe mfumo huu unamhitaji sana mwalimu kutumia teknolojia ya kisasa katika ufunzaji. Usishangae nikikwambia kuwa walimu wengi hawana mafunzo ya kisasa ya kompyuta. Zaidi ya hayo shule nyingi vilevile hazina tarakilishi. Baadhi yazo pia umeme haupo. Baada ya serikali ya uhuru kuahidi kuwapa Watoto vipakatalishi, je jiulize, ni wanafunzi wangapi hivi sasa ambao walipata vipakatalishi hivyo? Kando na hayo, wazazi wengi washalalamika kuhusu gharama kubwa ya vifaa ambavyo walimu huwatuma wanafunzi kuvileta shuleni. Huenda ikawa sababu ya wao kusema kuwa ni heri mfumo huo wa CBC ukaachiwa shule za kibinafsi.

Muda huo wote kila mtu pale tulipoketi alikuwa ametulia. Wapo waliotikisa vichwa kukubaliana naye Sumaku na wapo waliotikisa kukataa. Mara kijana mmoja tuliyemwita Sudi alisimama na kuzungumza. mawazo yake sudi ni kama yalikuwa ya kumpinga sumaku.

"Mtazamo wangu mimi ni kuwa mfumo wa CBC haufai kufutiliwa mbali. Itakuwa hasara kubwa kwa washika dau mbali mbali ambao wameekeza katika mfumo huu. Ikumbukwe kwamba imeigharimu serikali ya Uhuru pesa nyingi katika kujenga madarasa, kuwafunza walimu pamoja kuchapisha vitabu vya mfumo huu. Isitoshe kuutupilia mbali mfumo huu itakuwa sawa nakuwapotezea muda wanafunzi wa darasa la sita ambao kwa miaka sita wamekuwa wakisoma mfumo huu"

"Nakuunga mkono sumaku, alianza Dida. Kwanza sudi awazie tena udhaifu wa mfumo 8-4-4 ndipo awazie hayo. Kila mwanafunzi katika mfumo huu wa CBC ni mshindi. Hakuna kuwagawa wanafunzi katika makundi ya wajinga na werevu. Isitoshe, katika mtaala huu mpya, hakuna kurudia rudia madarasa kama ilivyo katika mfumo huo wa awali. Vile vile, mtaala wa CBC utawapa wanafunzi wa Kenya matumaini na fursa ya kuimarisha vipawa na uwezo wao. Ikumbukwe kwamba mtaala huu unasisitiza ukuzaji wa talanta za wanafunzi nchini tofauti na ule


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

wa 8-4-4. Pia, CBC humfunza mwanafunzi masomo ambayo tu yatamfaa maishani mwake. Lugha asili za wanafunzi pia zitakuzwa katika mfumo huu mpya.

Maneno yake Dida yalifunikwa ghafla na kelele za kumshangilia na kumsifu kijana huyu. Alipoona bado wanashangilia, aliinua mkono wake wa kushoto juu na kusema, "Basi ! Basi wanafunzi wenzangu, sina shaka ujumbe umeshafika.

***Maswali***

a) Ni mambo yepi yanayoleta utangamano baina ya vijana katika kundi hili chuoni?(alama 3)

i. ***Mambo yanayoleta utangamano utangamano baina ya vijana katika kundi hili***
ii. ***Masomo; wanafunzi hawa walitangamana chuoni kwa madhumuni yamasomo.***
iii. ***Haja ya kufanya utafiti kuhusu kazi mradi waliyopewa***
iv. ***Kuwepo kwa mtandao wa bure***
v. ***Mandhari ya kuvutia*** ***( 3x1)***

b) Eleza udhaifu wa mfumo wa 8-4-4 kulingana na kifungu hiki. (alama 5)

i. ***Udhaifu wa mfumo wa 8-4-4***
ii. ***Kuwatenga wanafunzi ; wale wanaojua na wale wasiojua.***
iii. ***Kuna kurudiarudia baadhi ya madarasa.***
iv. ***Hauimarishi talanta/ vipawa vya wanafunzi***
v. ***Baadhi ya masomo anayosoma mwanafunzi hayamfaidi maishani***
vi. ***Mtaala huu haukuzi lugha asilia za wanafunzi***. (5x1)

c) Jadili manufaa ya mfumo mpya wa elimu kulingana na Makala haya. (alama 5)

i. ***Manufaa ya mfumo wa CBC***
ii. ***Huimarisha vipawa/ talanta za wanafunzi***
iii. ***Masomo yote anayosoma mwanafunzi humfaa***
iv. ***Hukuza lugha asili***
v. ***Hakuna kurudia madarasa***
vi. ***Kila mwanafunzi ni mshindi.*** ***(5x1)***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

d) Kauli "upepo mwanana ulikuwa ukipita na kuzipapasa Ngozi zetu, " imetumia tamathali gani ya usemi? (alama1)

***Tashihisi/ uhuishaji/uhuishi (1/0)***

e) Eleza maana ya "tulinoleana bongo" kwa mujibu wa taarifa. (alama 1)

***Tulifahamishana/ tulielimishana (1/0)***

2.**UFUPISHO** **(alama 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:**

Kenya inakumbwa na hali ya hatari kuwahi kutokea msimu wa mvua ambayo imefanya serikali kuchukua hatua madhubuti za kuzuia maafa zaidi. Baada ya tathmini ya kina kuhusu hali ya hewa inayotarajiwa, serikali imelazimika kutangaza hatua za kuepusha vifo na uharibifu huku mvua ikitabiriwa kuendelea kunyesha na kimbunga kutarajiwa kutua Kenya kwa mara ya kwanza katika historia. Kimbunga hicho kitasababisha mvua kubwa, upepo mkali na mawimbi yenye nguvu na hatari, ambayo yanaweza kutatiza shughuli katika Bahari ya Hindi na makazi yaliyo karibu na pwani ya Kenya. Hali hii imechangiwa pakubwa na mabadiliko ya tabianchi.

Matukio ya hivi majuzi yamepima ustahimilivu wa nchi yetu wakati wa changamoto ambazo hazijawahi kutokea. Mvua imeendelea kusababisha mafuriko ambayo yameharibu miundomsingi. Vilevile, shughuli za uchukuzi zimetatizika katika sehemu zote za nchi baada ya barabara kuharibiwa na madaraja kusombwa na mafuriko.

Viwango vya maji katika mabwawa makuu ya 'Seven Forks' vimefikia kimo cha kihistoria huku mabwawa hayo yakitishia wanaoishi karibu na maeneo hayo. Kuna mabwawa 178 na vidimbwi vya maji katika ardhi ya umma na ya kibinafsi katika kaunti 33 ambayo yamejaa na kuwa hatari kwa wakazi walio maeneo yaliyo karibu. Vifo vya watu, kufurushwa kwa watu kutoka makwao na uharibifu wa mali umeshuhudiwa nchini.

Hatari nyingine imetokana na maporomoko ya ardhi na matope katika baadhi ya kaunti na wakazi wanaoishi katika maeneo hayo watahamishwa huku wanaoishi katika maeneo yasiyoratibiwa kama ya makazi kwa mfano kando ya mito, wakipewa ilani kuhama kwa kutambua hatari iliyopo.

Kwa sababu ya janga la mafuriko, wizara ya Elimu imeagiza kuahirishwa kwa tarehe ya kufunguliwa kwa shule zote nchini kwa muhula wa pili kwa muda usiojulikana. Pia, madhara ya mvua katika baadhi ya shule ni mabaya zaidi kiasi kwamba maisha ya wanafunzi yamo hatarini. Hatua ya kuahirisha ufunguzi wa shule hadi tarehe isiyojulikana imeibua mgawanyiko wa kitabaka huku watoto kutoka familia maskini, wengi wao wanaosomea shule za umma, wakiendelea bila masomo wenzao kutoka familia tajiri wakisoma kidijitali. Isitoshe,


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

bila tarehe mahususi za ufunguzi wa shule, ni vigumu kupanga masomo ya ziada wakiwa nyumbani. Hofu nyingine ni kuwa kukaa kwa muda mrefu bila kufanya chochote kunaweza kuwapelekea wanafunzi katika matumizi ya mihadarati na mimba za mapema.

Serikali imetangaza kuwa tarehe mpya za muhula wa pili kwa shule za msingi na za sekondari zitarekebishwa ili kufidia muda ambao ungepotezwa kwa kucheleweshwa kufunguliwa kwa shule. Tena, kutokana na mafunzo yaliyopatikana kufuatia janga la korona, wazazi wengi wanahimizwa kununua vifaa vya kidijitali vya kisasa ili kutumika katika masomo ya kidijitali.

Jeshi la Ulinzi la Kenya na Huduma ya Polisi zimeagizwa kutumia rasilmali, maafisa na vifaa vyao kuhakikisha wakenya wako salama. Wangeshirikiana na shirika la Huduma ya Vijana kwa Taifa na maafisa wa Utawala kushughulikia dharura ikiwemo kuokoa wote walio kwenye hatari.

Baraza la mawaziri limeagiza Wizara ya Fedha kutoa pesa za kusaidia kukabiliana na janga hili. Hata hivyo, kumekuwa na ukosefu wa uwazi katika utoaji wa fedha na hata misaada ambayo inakusudiwa kuendea walioathirika na vilevile haifikii wenye ulemavu-udanyanyifu katika mchakato mzima kuanzia kuwasilisha majina ya waathiriwa hadi ngazi ya malipo.

Idara ya utabiri wa hali ya Hewa nchini imewatahadharisha wakenya dhidi ya kuishi kando ya mito iliyofurika. Wanafunzi ambao tayari walikuwa wamefika shuleni walitakiwa kubaki shuleni na usimamizi wa shule ungewahifadhi na kuhakikisha usalama wao.

***Maswali:***

a) Huku ukirejelea aya nne za kwanza, eleza athari hasi za mabadiliko ya tabianchi. (Maneno 80) (alama 8)

Matayarisho

***i. Kenya inakumbwa na hali ya hatari kuwahi kutokea msimu wa mvua.***

***ii. Mvua kubwa imeendelea kusababisha mafuriko ambayo yameharibu miundomsingi.***

***iii. Shughuli za uchukuzi zimetatizika katika sehemu zote za nchi.***

***iv. Kuna hatari ya mabwawa kujaa na kuhatarisha maisha ya watu k.m vifo, uharibifu wa mali.***

***v. Maporomoko ya ardhi/matope kusababisha kuhamishwa kwa watu***

***vi. Uharibifu wa mali***

***vii. Vifo***

***vii. Kutatizika kwa shughuli za bahari (zozote 7x1=07)***



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

b) Fafanua masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tano za mwisho. (maneno 70) (alama 7)

Matayarisho

***i. Serikali imetangaza upya tarehe za kufunguliwa kwa shule.***

***ii. Wazazi wanahimizwa kununua vifaa vya kidijitali ili kuwezesha masomo ya kidijitali.***

***iii. Jeshi la Ulinzi na Huduma ya Polisi pamoja na Huduma ya vijana kushughulikia dharura ikiwemo kuokoa walio hatarini.***

***iv. Fedha kutolewa na wizara ya Fedha ili kusaidia kukabiliana na janga la mafuriko.***

***v. Kuna udanganyifu katika ugayi wa fedha/kutokuwa na uwazi katika utoaji wa fedha na hata misaada ambayo inakusudiwa kuendea waathiriwa.***

***vi. Idara ya Utabiri wa hali ya Hewa imewaonya watu dhidi ya kuishi karibu na mito.***

***vii. Wanafunzi waliomo shuleni wahifadhiwe mle na usimamizi wa shuleia kidijitali***

Teacher.co.ke

***(zozote 6x1=06)***

***1.Utuzaji***

***6h× ½ =3h***

***6s × ½ =3s***

***a) =07***

***b=06***

***utiririko =02***

***Majibu yaandikwe katika aya moja moja***

***kwa kila ziada ya maneno 10, ondoa alama 1***

**<u>SARUFI</u>**

a) Andika neno lenye (alama 1)

irabu ya nyuma, juu viringwa, kitambaza, irabu ya mbele juu tandazi, nazali ya ufizi, kipasuo ghuna cha kaakaa laini, irabu ya nyuma wastani

***Ulingo (1/0)***



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

b) Tofautisha sentensi zifuatazo kwa kuzingatia uamilifu (alama 2)

i. Mtahiniwa hajafuata maagizo yoyote-***arifu/taarifa***
ii. Pigia mstari majibu yako yote-***agizi*** ***(2x1)***

c) Ainisha viambishi katika neno: mmevipa (alama 2)

***i. M-nafsi ya pili wingi***
***ii. Me-hali timilifu***
***iii. Vi-yambwa***
***iv. P-mzizi***
***v. A-kiishio (2/0)***

d) Andika kinyume (alama 2)

Watoto wamemeza dawa wakakashifiwa.

***Watoto wametema dawa wakasifiwa. (2/0)***

e) Ainisha vielezi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Mwanafunzi hodari kabisa aliwapiku wachezaji wote michezoni.

***i. Kabisa-kielezi cha namna halisi***
***ii. Michezoni-kielezi cha mahali (2x1)***

f) Andika katika wingi. (alama 1)

Uyoga uliokuwa kwenye kasha umeoza.

***Uyoga uliokuwa kwenye makasha umeoza. (1/0)***

g) Tunga sentensi kuonyesha kitendo kinaendelea. (alama 1)

***Ninasoma. (1/0)***

h) Andika katika ukubwa. (alama 2)

Nyundo hii iliwaumiza watoto hawa na mtu mwingine. (2/0)

***Jundo / jijundo hili liliyaumiza matoto haya na jitu jingine.***

i) Andika sentensi upya ukifuata maagizo. (alama 2)

i. Kaumu alicheza mpira kwa niaba ya Jack. (anza kwa Jack)

***Jack alichezewa mpira na Kaumu.***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

ii. Waziri Ndiema aliteuliwa baada ya mtangulizi wake kujiuzulu. (Geuza neno lililopigiwa mstari kuwa nomino)

***Uteuzi wa waziri Ndiema ulitokana na kujiuzulu kwa mtangulizi wake.***
***Kuteuliwa kwa waziri Ndiema kulitokana na kujiuzulu kwa mtangulizi wake. (2x1)***

j) weka neno hili katika ngeli mbili tofauti. (alama 2)

Kucha -***KU na U-ZI*** ***(2x1)***

k) Yakinisha katika wakati ujao. (alama 2)

Mikunga hawajakuwa wakivuliwa kwa wingi.

***Mikunga watakuwa wakivuliwa kwa wingi. (2/0)***

l) Andika katika usemi taarifa. (alama 2)

"Ala! Mzee huyu ni mwenye imani hivi," Amani alishangaa

***Amani alishangaa kuwa mzee huyo alikuwa mwenye imani hivyo/vile. (2/0)***

m) Tambua aina za virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi hii. (alama 2)

Mwanamwali hodari ajabu alitembea kwa madaha kwenda kupokea tuzo lile.
***RV-Hodari ajabu***
***RH-kwa madaha*** ***(2x1)***

n)Ainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo: (alama 3)

Asha alimpikia shangazi yake wali mkavu kule kijijini.

***Yambwa tendwa-wali mkavu***
***Yambwa tendewa-shangazi yake***
***Chagizo-kule kijijini*** ***(3x1)***

o) Bainisha matumizi ya 'ki' zilizopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Kiatu ki chini ya meza lakini kitavaliwa na kijana anayetembea kijeshi.

**Ki**atu-***unominishaji*** ***1/2***
**Ki**-***kitenzi kishirikishi kipungufu 1/2***
**Ki**tavaliwa-***ngeli ya KI-VI 1/2***
**Ki**jeshi-***kielezi cha ki mfanano ½***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

p) Tambua aina za vishazi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Ingawa alifika mapema, hakumpata mwalimu.

***Kishazi huru-hakumpata mwalimu***
***Kishazi tegemezi-ingawa alifika mapema (2x1)***

q) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya koloni. (alama 2)

***Tulinunua: maembe, machungwa na mapera.***
***Alifika saa 4:15.***
***Tumaini: Je, umemuona mwalimu? (2x1)***

r) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia o-rejeshi ya mazoea. (alama 2)
Yule ambaye anatia bidii kazini ndiye ambaye anapandishwa cheo.

***Yule atiaye bidii kazini ndiye apandishwaye cheo. (2/0)***

s) Walakini ni kwa dosari /kasoro, tariki ni kwa ***barabara/njia/baraste*** na wazo ni kwa ***fikra.*** (2x1) (alama 2)

t) Changanua kwa njia ya visanduku/jedwali. (alama 4)
Kijana yule hodari amefuzu vyema.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ***S*** | | | | |
| ***KN*** | | | ***KT*** | |
| ***N*** | ***V*** | ***V*** | ***T*** | ***E*** |
| ***Kijana*** | ***yule*** | ***hodari*** | ***amefuzu*** | ***vyema*** |

(8x1/2)

**ISIMUJAMII**

… Watu wa kaunti ya Maji Mazuri wamesahaulika kabisa. Ningependa kuelezwa kinagaubaga kama hawa ni Wakenya au la. Order! Order! Mheshimiwa Tumbili.

a) Bainisha sajili hii. (al. 2)

***Sajili ya bungeni-mheshimiwa (2x1)***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

b) Fafanua zozote tatu zinazojitokeza katika Makala haya. (al. 3)

***1. Msamiati wa kisheria k.v katiba***
***2. Lugha ya maelezo. hutumiwa ili kutoa maelezo kamilifu na yanayoeleweka.***
***3. Lugha ya adabu na heshima huzingatiwa ilikudumisha heshima katika bunge.***
***4. Urudiaji mwingi ili kusisitiza hoja.***
***5. Kukatizana kalmia.unapopinga hoja ya mzungumzaji.***
***6. Upishanaji zamu kudhibitiwa na spika; ndiye aamuaye nani azungumze na vipi.***
***7. Viziada lugha.Kushangilia hoja kwa kupigisha miguu chini***
***8. Fomula maalum ya kuanza na kutamatisha mazungumzo mf asante bwana spika kwa fursa hii.***
***9. Mbinu rejeshi kwa wingi kurejelea tukio lililotendeka.***
***10. Lugha ya taifa au rasmi ni muktadha rasmi.kiswahili au kingereza.***
***11. Kiwango Fulani cha utani (4x1)***

2. Fafanua kwa kutoa mifano mwafaka mambo manne yanayosababisha watu kufanya makosa wanapotumia lugha ya kiswahili.

***i) Athari za lugha ya kwanza – mbamba badala ya baba/lara badala ya raha***
***ii) kutozielewa kaida za matumizi ya lugha- babu/nyanya kumsalimu mjukuu "shikamoo"***
***iii) uhamishaji wa kaida za lugha moja hadi nyingine- kunywa sigara badala ya kuvuta sigara***
***iv) ujumlishaji wa kanuni za kisarufi – watu wasita badala ya watu sita,***
***v) upungufu wa viungo vya kutamkia – kukosa meno/kukatika midomo/kigugumizi***
***vi) hali ya mtu anapozungumza – mlevi hufanya makosa kiholela***
***vi) kuzungumza harakaharaka –***
***vii) makosa ya kimakusudi –***
***viii) kutoimudu lugha vilivyo ( za kwanza 4 x 1) (4x1)***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes